

80 YA FIMBO

Utenzi wa kusherehekea miaka 80 ya kuzaliwa ya Prof. Gamaliel Mgongo Fimbo (Kuzaliwa 08/08/1943). Boardroom, A.B Weston Building.

1. Ee Rabana mwenye heri
Na neema utitiri
Mtoa afya buheri
Leo umetupatia
2. Sio kwa zetu hesabu
Pendo lako ni jawabu
Uliyetupa sababu
Pamoja tumejongea
3. Tunazikumbuka zama
Ukoloni huko nyuma
Kwa macho tumezisoma
Fimbo zilituletea
4. Kabla TANU kuundwa
Vita pili ikidundwa
Makalu haujapandwa
Bongo mwamba alitua
5. Alishuka Magharibi
Kwenye asali vinubi
Kilimoni si udobi
Safari alianza
6. Mbambe Tino Kalungwana
Mwalimu pika vinona
Umahiri aliona
Fimbo pepa kupasua
7. Kitunda una alama
Tabora walikusoma
Mzizima kuzizima
Kufupi ulipania
8. Sita tisa na shahada
Kitivo ukawa kada
Kwako nyumba ya ibada
Mkongwe ulosalia
9. Wewe kwetu ni alama
Nembo utendaji mwema
Nyendo zetu kujipima
Histori kurejea
10. Nyerere umemuona
Na Mwinyi umemfana
Benja Kikwete vijana
TIRA ulisaidia
11. Kabla ya manyang'au
Nguo mitumba za Macau
Mbio Filbert Ba-u
Wasomi walikujua
12. Hata wasojulikana
Mara chawa waso mana
Upepo vumbi Corona
Kipi usichokijua?
13. Mahakama Mwalusanya
Kwa Vitabu hukuhanya
Abualy, Lugora-nya
Mtobesya anajua
14. Muumini wa heshima
Watumishi usalama
Kuenenda kwa hekima
Mawazo kibishania
15. 80 si mbovu
Myaka ya wenye nguvu
Kilele cha ukomavu
Busara kutuzidia

16. Mzee wetu kijana
Japo uvae fulana
Kaputula la kichina
La Marx ulikimbia
17. Ni Russia Ukraine?
Msimbazi, wa Jangwani?
Siulizii Imani
Nyumba yako najjua
18. Kwetu tuna mtihani
Swali sasa na zamani
Kuna vyumba vi gizani
Taa mliziondoa?
19. Tupo twaranda nyikani
Nanyi wachora ramani
Paka tuzame shimoni?
Msisite kuongea
20. Imegeuka shilingi
Vimeongezwa vingi
Taaluma si msingi
Twabagazwa na wambea
21. Miluzi mekuwa mingi
Na uongo nao mwingi
Ujuzi sio msingi
Wafuasi waongea
22. Tumekaa hapo kando
Ya bandari na magendo
Mepesi na ya mgando
Kulia twajizuia
23. Umetundika daruga
Benchi unapiga soga
Ona tunavyoupiga
Tisini tunatoboa?
24. Ibaki kwetu wajuzi
Imara kufanya kazi
- Mtaji wa kumbukizi
Tumefika twapitia?
25. Wanatung'ong'a la saba
Wachekeshaji si haba
Hatuna chetu kibaba
Hasara tumewatia?
26. Yamenitoka mlumbi
Dhati si uchakubimbi
Umeyashinda mawimbi
Kongole nakutolea
27. Zinaniisha na tenzi
Kwa yote sitokuenzi
Ukiwa hai mpenzi
KITABU twasubilia
28. Tunakuombea mengi
Uongezwe myaka mingi
Ya heri sio vingi
Tuifurahie MIA
29. Pepo njema zikutii
Kwa afya uwe Nabii
Yote mema yakuswii
Visuti kutopungua
30. Nimezitungua tenzi
Sasa nagota ujenzi
Namuomba MWENYE-ENZI
Ushinde vibirikizi.